**Maswali na Majibu**

1. Neno kanisa kwa Biblia lina maana gani?
*Wakristo wanaokutano pamoja, sio jingo wanalokutania.*
2. Wakristo wa kwanza walikutania wapi?
*Kwa nyumba ya mmoja wa washiriki.*
3. Wasimamizi wa kanisa walifanya nini?
*Panga kazi, angalia washiriki, hudumia kanisa.*
4. Wasimamizi wa kanisa walikuwa watu wa namna gani?
*Watu waaminifu, tena watu waliokuwa na ufahamu wa Injili.*
5. Wanaume walikuwa wakifanya nini kwa kanisa ya kwanza?
*Walisaidia kufundisha na kuhubiri, soma Biblia na kuomba.*
6. Wanawake walifanya nini kwa kanisa ya kwanza?
*Walilinda maskini na wagonjwa, walikaribisha Wakristo kwa nyumba zao na walifundisha watoto juu ya Mungu.*
7. Wakristo wa kwanza walifanya nini kila siku?
*Walijaribu kufurahisha Mungu, waliomba, soma Biblia na kujitenga na maovu.*
8. Wakristo wa Kwanza walifanya nini walipokuwa wakikutana pamoja?
*Walimega mkate na kukunywa divai wakikumbuka Yesu kama dhabihu.*
9. Mfalme Constantino alilazimisha Warumi wafanye nini?
*Aliwalazimisha wote wawe Wakristo.*
10. Hii ilikuwa na matokeo gani kwa kanisa la Wakristo?
*Hii ilisababisha kuleta dini kafiri kwa mafundisho ya Ukristo na ikabadilisha ukweli wa Mungu na kuingiza mafundisho ya watu.*

### Mistari ya kukariri

Waefeso 4:4 – 6 Wagalatia 1:8 1 Timotheo 2:5

### Mazungumzo

Inatosha kupata wokovu kwa kuamini Injili ya Mungu ya kweli? Zungumza juu ya mafundisho yasiyo ya kweli yenye iko kwa makanisa. Injili ya kweli inatufundisha kwamba tuamini nini?

### Kuandika

Andika vile makanisa ya kwanza ya Wakristo yalikuwa.

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 42 Makanisa za kwanza za Wa-

**SOMA Matendo 2:41 – 42; 1 Wakorintho 11:23 – 26; Wagalatia 1:6 – 9; Waefeso 4:4 – 6.**

**SOMO**

Makanisa za Wakristo za kwanza, zilikuwa ni vikundi vya Wakristo waliokuja pamoja kuabudu Mungu. Wakristo wa kwanza walikuwa Wayahudi na Wamataifa, wanaume na wanawake, mabwana na watumwa. Upendo wao kwa Yesu uliwasaidia wasiwe na utofauti wa utamaduni wala vyeo. Wakristo wa kwanza wote waliamini ujumbe wa Injili moja iliyofundishwa na wanafunzi. Walikuwa na tumaini moja ya wokovu katika Yesu Kristo. Wote walibatizwa ndani ya Yesu. Wote walikuwa ndugu na dada wa Yesu na kuwa baadhi ya familia ya Mungu.

Mafundisho ya muhimu ya Wakristo wa Kwanza ilikuwa kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu. Yesu alizaliwa na bikira Mariamu na akaishi maisha makamilifu. Alikufa na kufufuka kuwa hai tena. Sasa ana maishi ya milele na ako na Mungu mbinguni. Yesu alitimiza ahadi zenye Mungu alifanya na watu wake kwa Agano la Kale. Yesu alitoa uhai wake uliokuwa kamilifu ili watu kutoka mataifa yote wasamehewe dhambi zao na wawe na tumaini la uzima wa milele wakati Yesu atakuja kusimaisha Ufalme wa Mungu hapa duniani. Hao Wakristo walifunza kwamba, watu watubu na wabatizwa ndani ya Yesu Kristo. Lazima wabadilishe maisha yao na waishi maisha ya kumpendeza Mungu wala sio kujipendeza wao wenyewe. Wakristo wa kwanza wote waliamini mafundisho yote ya Ukristo.

Wakristo wa kwanza walikuwa wakikutania kwa nyumba ya mmoja wao. Hivi vikundi vya Wakristo vilikuwa vya watu wachache. Neno ‘kanisa’ kwa Biblia linamaanisha Wakristo waliokutana pamoja sio jingo lenye walikutania. Haikukuwa na maana walipokutania. Ilikuwa ya maana kufundishe neno la Mungu la kweli na waabudu Mungu kwa njia inayompendeza.

Paulo alihubiri Injili na kubatiza watu wengi. Alisimamisha makanisa ya Wakristo katika eneo lote la Milki ya Warumi. Mara nyingi Paulo alikaa na kanisa moja kwa muda kuona kwamba waliisimamia vizuri kabla aondoke na kuendelea na safari yake.

Wasimamizi walichakuliwa ili wasimamie mipango ya kanisa. Hawa wasimamizi walikuwa watu waaminifu na walikuwa wawe na ufahamu wa Injili. Kawaida walikuwa watu wazee. Wazee hawa waliona kwamba mipango inaendeshwa vizuri. Huduma ya kanisa ilikuwa ya kuabudu Mungu; kila kitu kilikuwa kifanyike kwa utaratibu na Mungu apewe utukufu. Wasimamizi walisaidia kila muumuni wa kanisa. Wasimamizi walihudumia kanisa. Hawakukuwa eti ni wamaana kuliko wenzao. Walichakuliwa kusaidia kanisa. Hawakulipwa kwa hiyo kazi.

Watu wote walisaidiana kwa kazi ya kanisa. Kila mshiriki alifanya kazi yenye aliweza. Wanaume walisaidia kufundisha na kuhubiri. Walisoma Biblia na kuomba. Wanawake walisaidia waliokuwa wagonjwa na maskini. Walisaidia Wakristo waliokuwa wakiishi kwa nyumba zao. Walifundisha watoto juu ya Mungu.

Yesu alikuwa ameamrisha wanafunzi wake kukumbuka kifo chake kwa kumega mkate na kunywa divai. Wakristo wa kwanza walifanya hivi kila juma. Walikumbuka vile Yesu alijitoa kama dhabihu kwa ajili yao. Walishukuru Mungu kwa sababu ya huo wokovu kupitia kwa Yesu. Walitubu dhambi zao na kuahidi kujaribu sana ili wafurahishe Mungu. Wakristo walimega mkate kukumbuka mwili wa Yesu uliotezwa msalabani. Walikunywa divai kukumbuka damu ya Yesu iliyomwagika kwa ajili ya dhambi zao. Wakristo walisoma Biblia. Walihimizana kwa hali zote. Waliimba nyimbo na kuomba pamoja. Mkutano wao haukuwa wa gharama nyingi. Hawakuwa na mtu wa kipekee wa kuongoza ibada. Wanaume wowote walioweza, wangesaidia kusoma, kunena vile Biblia imesema na kupeana maombi. Hakukuwa na nguo za kipekee au utamaduni uliotatanisha. Wakristo wa kwanza walifanya kazi pamoja wakihudumia Mungu na kumwaabudu.

Wakristo wa kwanza walikuwa kama jamii moja kubwa. Walikuwa wote ndugu na dada katika Yesu. Walisaidiana wenyewe kwa wenyewe. Wengine wao waliuza mashamba na hata nyumba zao ili watumia hizo pesa pamoja na wasiojiweza. Paulo alichangisha pesa kutoka kwa makanisa aliyosimamisha ili awapelekee Wakristo wa Yerusalemu.

Wakristo hao walikuwa na nidhamu ya juu. Hawakujihuzisha na tabia za watu waliokuwa wakiishi karibu nao. Wakristo walijitenga na maovu ya dunia waliyoishi. Waliishi maisha yasiyokuwa na gharama nyingi. Walijaribu kumpendeza Mungu kuliko wao wenyewe. Waliomba Mungu kila siku. Walisoma na kuwa na mazungumzo juu ya neno la Mungu. Walifurahia kukaa pamoja na kujadili juu ya wokovu mkuu yenye Mungu aliahidi kuwapa wakati Yesu atarudi hapa duniani kusimamisha Ufalme wa Mungu. Jambo lililokuwa la maana sana kwa hao Wakristo wa kwanza ni tumaini walilokuwanalo ni wokovu wa Mungu katika Yesu. Inabidi iwe ya muhimu hata kwa sisi.

Paulo na wanafunzi walifundisha kwamba ujumbe wa Injili ya Mungu usibadiliswe. Mafundisho ya Biblia ni neno la Mungu. Tusisikilize mafundisho ya watu badala ya mafundisho ya Mungu. Ujumbe wa Injili si ngumu na inaeleweke vizuri. Mawazo na mafundisho ya watu imefanya mafundisho ya Wakristo itatanishe. Lazima tubaki kwa mafundisho ya kweli ya Wakristo wa kwanza.

Watu wa Mataifa walikuwa na dini zao za wakafiri. Wakristo wa kwanza wengine walipenda mafundisho ya hawa watu na walikuwa wameamini kabla ya kuwa Wakristo. Walitaka kutumia hayo mafunzo mengine ya hizo dini. Walianza kuongeza hayo mafundisho kwa Injili ya Wakristo. Hii ilileta shida nyingi sana. Paulo aliandikia makanisa yenye alisimamisha kwamba ni vibaya kuleta mafundisho ya watu kwa ukweli wa Mungu.

Baada ya miaka karibu 300, tangu kusimamisha makanisa ya Wakristo, kulikuwa na mfalme wa Roma aliyeitwa Constantino. Constantino alifanya dini ya Kikristo kuwa dini rasmi ya kitaifa ya Roma. Alilazimisha kila mtu awe Mkristo. Kuamua kuwa Mkristo ni jambo la maana sana. Inatakiwa uwe uamuzi wa maisha na uahidi kujitolea kupea Mungu maisha yako yote. Ni makosa kulazimisha mtu kuwa Mkristo. Inatakiwa mtu mwenyewe aamue.

Warumi walizoea kuabudu miungi wengi. Walikuwa na karamu nyingi na kufurahia wakati mwingi kuwa na ghasia kwa ajili ya kulewa divai na wanawake. Warumi hawakutaka kubadilika wawe Wakristo. Constantino alilazimisha Warumi wajiite Wakristo. Waliendelea kuwa na desturi na sherehe zao za ukafiri, ingawaje walijifanya kwamba wanatimiza sherehe za Wakristo. Kwa mfano Krismasi ilikuwa siku kuu ya wakafiri.

Pia, Warumi walitaka kutimiza siku kuu za dini na imani yao. Constantino aliwalazimisha kuwa Wakristo. Lakini hangewalazimisha kuamini mafundisho ya Wakristo. Baada ya muda hawa watu waliingiza imani yao kwa mafundisho ya Kikristo. Waliongeza mafunzo ya dini ya Kigiriki na Kirumi kwa yale ya Kikristo. Haya mafundisho yasiyo ya kweli bado ingali kwa madhehebu nyingi mpaka sasa. Hayo si mafunzo ya Mungu wala Biblia.

Paulo alifundisha kwamba ni muhimu sana kuamini mambo yenye Mungu ametufundisha. Tuamini mafundisho ya Mungu lakini sio ya watu. Hata sasa bado ni muhimu kwetu. Kila mara tuwe tukilinganisha mafundisho yenye makanisa yanafundisha na lile Neno la Mungu linasema. Kuna Ukweli moja tu. Ona kwamba unaamini ukweli wa mafundisho ya Wakristo.